



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ مَأْمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لِيَسْتَخْلِفُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَفْسَنَ خَلْفَهُمْ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يَكُنْ لَّهُمْ لِئَلَّا يَرَوُنَ مُلْكَنَا مُلْكَنَّهُمْ وَلَمْ يَكُنْ لَّهُمْ مِنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَنَّهُ
يُعْذِّبُونَهُمْ لَا يُشْرِكُونَ بِهِ شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بِهَذَا ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ

Toleo: 05 / 1446 H

Jumamosi, 2 Rabi' II 1446 H

05/10/2024 M

Taarifa kwa Vyombo vy ya Habari
Vilio vya Kuficha Mauaji ya Halaiki

(Imetafsiriwa)

Wanaotetea mauaji ya halaiki na wavezeshaji wao wasio na haya katika vyombo vy ya habari na siasa wamezusha raundi nyingine ya msukosuko wa kimakusudi unaozunguka mukutano uliopendekezwa huko Lakemba, ukiangazia kampeni ya mwaka mzima ya mauaji ya halaiki nchini Palestina.

Hizb ut Tahrir/Australia ingependa kueleza hadharani kwamba dhana na uongo unaoenezwu na wafusi wa Kizayuni kuhusiana na waandaaji wa mukutano huo, bora zaidi, wamepewa taarifa potofu na baya zaidi, ni kwa nia mbaya. Inashangaza kwamba wanasiwa daima wanatoa wito wa kuwepo kwa uwiano wa kijamii lakini hawana kusita katika kukubali simulizi za uongo - kueneza habari potofu katika mchakato huo na hatimaye kuhujumu "mshikamano wa kijamii" wanaoupigia debe.

Ulimwengu unatazamiwa kuamini kwamba hatari kubwa zaidi hailetwi na wale wanaotekeleza mauaji ya halaiki, bali wale wanaoyavutia. Tunaulizwa kuamini kuwa ni kutojali kukusanyika siku fulani, lakini sio kupiga mabomu, kuua siku hiyo hiyo.

Kamjeni hii ya hivi punde ya propaganda inazidi kuchochea moto wa chuki dhidi ya Uislamu—sio kuridhika na kuwadhalilisha Wapalestina wote, lakini pia kuwalenga wale wanaokusanyika kutafakari maumivu yao wakati wa mauaji ya halaiki.

Je, ni kwa jinsi gani madai na maonyo kuhusu kusambaratisha mshikamano wa kijamii yanaweza kuchukuliwa kwa uzito kutoka kwa wale wanaohalalisha, kwa kila njia, kuichana miili ya wanadamu?

Madai haya hayana msingi, yamepotoka, ya uongo. Lakini ulimwengu tayari unajua hilo.

Ni wakati sasa wa serikali ya Australia kukiri hilo pia.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir
Australia**

Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:

Tovuti: www.hizb-ut-tahrir.dk

Pepe: info@hizb-ut-tahrir.dk

www.hizb-ut-tahrir.org

Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:
www.hizb-ut-tahrir.info